

TANGAZO KWA WAFANYABIASHARA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA, KATIKA KUHAKIKISHA HUDUMA ZINAWAFIKIA WAFANYABIASHARA KWA URAHISI NA KUMWONDOLEA MTEJA KUFIKA MAKAO MAKUU YA WILAYA NGUDU MJINI KUCHUKUA FOMU YA MAOMBI YA BIAHARA, IMEAMUA KUWEKA KATIKA TOVUTI YA HALMASHAURI FOMU ZOTE ZA MAOMBI YA LESENI ZA BIAHARA ILI MFANYABIASHARA ANAYEHITAJI KUENZISHA BIAHARA APAKUE (DOWNLOAD) FOMU YA BIAHARA HUSIKA NA KUISAINISHA KWA AFISA MTENDAJI WA KIJJI NA AFISA AFYA WA KATA/TARAFU HUSIKA. MAELEKEZO ZAIDI:-

A. WAFANYABIASHARA WAPYA:

1. Ingia katika tovuti ya Halmashauri: www.kwimbadc.go.tz
2. Nenda sehemu ya nyaraka
3. Chagua aina ya fomu unayohitaji; Mfano fomu ya leseni ya Vileo/Pombe
4. Pakua (download) fomu husika
5. Nenda Ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji sainisha eneo husika
6. Biashara za Vileo, Migahawa, Nyumba za Kulala Wageni, Dawa za Binadam, Pembejeo na biashara nyingine zinazohitaji masharti ya kiafya zaidi; fomu yake lazima isainiwe eneo la Afisa Afya wa Kata husika au Tarafa endapo Afisa Afya wa Kata hayupo.
7. Baada ya fomu kusainiwa ngazi ya kijiji na kata, Mfanyabiashara afike Ofisi ya Biashara kwa ajili ya kuwasilisha ombi lake
8. Mfanyabiashara ataenda Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa ajili ya kupata Nambari ya Mlipa Kodi (TIN). Kumbuka: ili upate TIN lazima uwe na Nambari ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA).
9. Baada ya Mfanyabiashara kupata TIN, atarudi Ofisi ya Biashara kwa ajili ya kulipia ada ya leseni na kupatiwa leseni husika.

B. WAFANYABIASHARA WA ZAMANI WANAOHUISHA BIAHARA ZAO (LICENSE RENEW) FIKA:-

1. Leseni ya biashara iliyomaliza muda wake
2. Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi (Business Tax Clearance) kutoka TRA
3. Ada ya leseni ya biashara husika kwa Mujibu wa Mwongozo wa Ada/Maelekezo yaliyotolewa na Ofisi wakati wa Ukaguzi wa Leseni za Biashara

KWA MAWASILIANO NA KUPATA ELIMU YA BIAHARA ZAIDI;

1. Barnabas Kulwa – Afisa Biashara: 0756 671821 au 0787 244927
2. Victoria Kidolezi – Afisa Biashara: 07855 737451
3. George Masaki - Afisa Biashara: 0757 505953